Jarida la Shirika la Uboreshaji Mifereji ya Asili na Uhifadhi wa Mazingira (TIP)

Maendeleo ya TIP

Toleo la 9 2006



# MCHEZO WA ENEO BONDE

- Mchezo wa eneo bonde ni nini?
- Jinsi unavyochezwa
- Manufaa ya mchezo

## Mchezo wa eneo bonde ni nini?

Ni mchezo ambao hutumika kuhamasisha mahusiano mazuri katika matumizi ya maji. Ni chombo ambacho kinaonyesha mfano halisi wa eneo bonde la mto kwa kuonyesha ukanda wa juu na ukanda wa chini wa mto. Watumiaji maji wa ukanda wa juu wa mto huonekana kupata nafuu kubwa kuliko walio katika ukanda wa chini. Tofauti hii husababisha mgawanyo usio sawa wa maji kati ya watumiaji wa ukanda wa juu na ukanda wa chini. Hii husababisha kuanza kwa migogoro ya maji. Pia mchezo huu huchezwa ili kufanikisha tafiti na kuwezesha kutoa maamuzi sahihi kuhusu watumia maji.

Kama inavyoonekana katika picha, mchezo huu ni ubao mkubwa kwa upande mmoja ukionyesha mwinuko na upande wa pili ukionyesha eneo bonde na maeneo oevu. Mto hutiririka kutoka upande mmoja kwenda mwingine ukiwa na baadhi ya mabanio kwa ajili ya mifumo mbali mbali ya umwagiliaji katika viwango tofauti. Baadhi ya mifumo ya umwagiliaji inanufaika zaidi kutokana na kuwa ukanda wa juu wa mto kuliko mifumo mingine ya umwagiliaji iliyo katika ukanda wa chini wa mto. Mto hutiririsha maji wakati gololi za kioo zinapoachiwa kutoka juu na kuelekea chini ya ubao. Gololi hizi hutumika kuwakilisha maji.

> mahusiano mazuri kati ya watumia maji wa ukanda juu na wa chini, ni utatuzi wa migogo ya maji katika eneo bonde la mto

## Jinsi unavyochezwa

Mto utakuwa unapitisha maji pale ambapo gololi zitakapomwangwa kuelekea upande wa chini wa mto. Gololi hutumika huwakilisha maji. Washiriki hukinga gololi kwa kutumia vibao vidogo (mfano wa banio) na kuzielekeza katika mashamba ya umwagiliaji ambapo zitatua kwenye vishimo vidogo vilivyopo kwenye mashamba hayo vikiwakilisha kiasi cha maji kinachohitajika katika shamba husika. Picha inaonyesha vibao vinavyoteka gololi kwa urahisi – hivi huwakilisha mabanio yaliyoboreshwa. Baada ya mchezo washiriki watakuwa na ufahamu wa nini kinachotendeka, nini kinachotakiwa kulengwa na ufumbuzi gani unaoweza kufikiriwa. Siku ya pili itakuwa ya kufuatilia nini washiriki wamejifunza kutokana na mchezo na kuweka pamoja mawazo mbalimbali



Ubao wa mchezo wa eneo bonde

yatakayosaidia kuboresha usawa katika ugawaji maji. Siku zote mbili zinahitaji maandalizi mazuri ili kufanikiwa.

## Manufaa ya mchezo

1. Mchezo husaidia wanafunzi na watafiti wa matumizi bora ya maji kufundisha matumizi sahihi ya maji.
2. Husadia watumia maji wadogo kuwezesha kuwa na maamuzi kulingana na mgao wa maji. Mchezo huu pia husaidia watafiti kugundua utatuzi ya migogoro ya maji iliyopo.
3. Husaidia watoa maamuzi wa ngazi ya juu kudhihirisha matatizo yanayowakabili watumia maji wadogo na matokeo hasi yatokanayo na uamuzi waliojichukulia.
4. Mchezo husaidia taasisi za ngazi ya juu pamoja na watumia maji kuwa na upeo mkubwa wa uelewa kuhusu ushirikiano, utayari na jitihada zinazohitajika kutunza maji katika eneo bonde la mto.

## "Yaliyomo"

Mkutano wa wadau wa soko la zao la Mahindi........................... *ukurasa wa 2*

Unafahamu nini kuhusu Ukimwi na Virusi vya Ukimwi ...........*ukurasa wa 2*

Mafanikio ya Utafiti shirikishi wa masoko Arumeru .........................*ukurasa wa 3*

Wakulima wa Arumeru waomba mafunzo ya usindikaji........*ukurasa wa 3*

Wanawake katika maendeleo......................*ukurasa wa 3*

Mkulima wa Mwanga aishukuru TIP..................................*ukurasa wa 3*

Ukarabati wa ndiva waongeza uzalishaji wa tangawizi .....*ukurasa wa 3*

Kutumia teknolojia rahisi kwaongeza uzalishaji wa mazao .........*ukurasa wa 3*

Jinsi uboreshaji wa mifereji asili ilivyoboresha...................*ukurasa wa 4*

# Mkutano wa wadau wa soko la zao la Mahindi wilaya ya Arumeru

Wakulima wa wilaya ya Arumeru wana uwezo wa kuzalisha kwa kiasi kikubwa lakini wanakabiliwa na soko la uhakika litakalo wapa faida. Wengi wao huzalisha kiasi kidogo kwa kuuza na hujikuta wakiwauzia wafanyabiasha wachuuzi wa mazao kwa bei ya chini ukilinganisha bei ya jumla. Uwezo wa kusimamia bei inayolipa kwa mkulima mmoja mmoja ni vigumu inambidi kukubali bei anayotoa mfanyabiashara.

*Nini kifanyike?*

Wakulima wakubwa hawakabiliani na matatizo kama haya. Wana uwezo wa kuzalisha kila zao kwa kiasi kikubwa na katika kiwango kinachokubalika. Kwa sababu hii hawapati ugumu kutafuta wanunuzi na hupata bei nzuri kwa mazao yao. Kinachotakiwa kwa wakulima wadogo kuweza kukabiliana na hali hii ni kuungana na kuunda umoja wao. Kufuatia mchanganuo wa mtiririko wa soko la zao la mahindi, ulifanyika mkutano wa wadau wa zao la mahindi tarehe 31 Januari 2006 katika ukumbi wa hoteli ya Golden Rose, Arusha.

Madhumuni ya mkutano yalikuwa:

i. Kuhusisha wadau wote wa soko la zao la mahindi kukaa na kujadiliana changamoto zinazowakabili na kutoa ufumbuzi.
ii. Kuimarisha hali ya shinda shinda katika biashara ya zao la mahindi kwa wadau wote
iii. Kuwawezesha wakulima wadogo kujiunganisha na masoko ya uhakika

Jumla ya washiriki 35 walihudhuria mkutano huo wakiwamo wawakilishi kutoka:

i) Kenmillers LTD – Wasindikaji wa mazao ya mahindi
ii) Banki ya CRDB bank – tawi la Arusha
iii) Taasisi ya utafiti wa kilimo Seliani (SARI)
iv) Wazalishaji wa mbegu
v) Waliwakilishi wanne wa wakulima kutoka kila kata za: King'ori, Makiba, Maroroni, Bwawani, Ilkiding'a, Nkoarisambu na Nkoaranga.
vi) Maafisa ugani
vii) TCCIA - tawi la Arusha

*Fursa iliyopo*

Wasindikaji waliwajulisha wakulima kwamba uhusiano kati ya wasindikaji na wazalishaji upo kwa maana kwamba, wazailishaji ndio wauzaji na wasindikaji ni wanunuzi. Kuna soko la uhakika la zao la mahindi kwenye viwanda vya kusindika mahindi. Viana uwezo wa kuchukua tani 75 kwa wiki. Bei wanayolipa inategemea na hali ya soko kwa wakati huo. Kuna changamoto zinazosababisha wasindikaji kununua mahindi kutoka kwa mtu wa kati na si kwa mkulima moja kwa moja. Suluhisho la haya yote liko mikononi mwa wazalishaji

*Ushauri kwa wakulima.*

Maafisa ugani waliwashauri wakulima kununua mbegu bora pamoja na viuatilifu na kudai atakabadhi. Inapotokea tatizo lolote watakuwa na uwezo wa kumchukulia taratibu za kisheria muuzaji. Wanatakiwa pia kuchukua vipeperushi vinavyoelezea matumizi ya dawa hiyo au pembejeo yeyote walioinunua. Wakulima wanasisitizwa kufuata ushauri kuhusu utunzaji wa shamba na mbinu bora za kilimo.

Watafiti waliwashauri wakulima kutumia vipimo sahihi vya viuatilifu ili kuzuia wadudu wasiweze kujijengea kinga, kwani ni gharama sana kuzalisha dawa nyingine ya kuua wadudu ambao walishajijengea kinga ya kupambana na dawa. Wadudu waharibufu hujijengea kinga pale ambapo kipimo cha dawa hakikutumika ipasavyo.

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Seliani (SARI), iliwashauri wazalishaji kulima mahindi yenye lishe bora (*Quality Protein Maize).* Hii itasaidia kuboresha afya za walaji kwa sababu mahindi haya yana viinilishe vyote vinavyotakiwa katika mwili wa binadamu.

Benki ya CRDB iliwashauri wakulima kuomba mkopo kutoka benki. Wajiunge katika vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS) vilivyosajiliwa. Benki inatoa mafunzo bila gharama kwa vyama ili kuviimarisha.

## Unafahamu nini kuhusu Ukimwi na Virusi vya Ukimwi (VVU)? Jipime uelewa wako kwa kutumia maswali yafuatayo?

*"Bado kuna uelewa mdogo kuhusu maambukizi ya VVU kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Ukiwa na ufahamu, utaepuka kuambukizwa VVU kama hujaathirika, pia kutoambukiza kama umeathirika"*

1. Nani anaweza kupata maambukizo ya VVU?
   A. watu wasio kwenda kwa daktari mara kwa mara.
   B. ambao hawakumaliza elimu ya msingi
   C. yeyote ambaye ameshiriki ngono bila kutumia kinga au kuchangia vitu vyene ncha kali.
2. Mtu anaweza kuambukiza VVU pale tu mwili wake utakapoonyesha dalili za kuathirika na kinga yake ya mwili inapokua imeshuka.
   Kweli.
   Si Kweli
3. Ukimwi ni kati ya magonjwa yanayo ambukizwa kwa njia ya kujamiiana. Ukiwa na ugonjwa wa zinaa, uwezo wa kuambukizwa ukimwi kwa njia ya kujamiiana uko katika kiwango gani?
   A. Juu.
   B. Wastani.
   C. Chini.
4. Rafiki kakualika nyumbani kwao kwa chakula cha jioni na unafahamu kuwa mama yake ameathirika. Uwezekano wa wewe kuambukizwa ukimwi utakapokula chakula kilichotayarishwa na mama huyu upo katika kiwango gani?
   A. Juu.
   B. Chini.
   C. Hakuna.
5. Je vidonge vya uzazi wa mpango, vinazuia maambizi ya ukimwi?
   Kweli
   Si Kweli
6. Ulevi na madawa ya kulevya havitoi msukumo wa matamanio ya kujaamiana?
   Kweli
   Si Kweli.
7. Umesikia kuwa mtu aliyekaa kiti cha pembeni yako kwenye basi ana maambukizo. Je hatari ya wewe kupata maambukizo kutoka kwa mtu huyo ipo katika kiasi gani?
   A. Hakuna.
   B. Juu.
   C. Chini.
8. Unaweza kufahamu kwamba umeambukizwa kwa:
   A. Kupima damu.
   B. Kupiga eksirei.
   C. Kufanya uchunguzi wa ngozi.
9. Katika vipimo mtu anaweza kuonekana hajapata maambukizo lakini ni muathirika wa ukimwi.
   Kweli.
   Si Kweli.
10. Kama kuna mtu unamjua ameathika na ukimwi, utamsaidia kwa kufanya nini?
   A. kuwaeleze watu wamuepuke.
   B. kukaa mbali naye
   C. kutafuta njia sahihi za kukuwezesha kutoa msaada unaohitajika.

Majibu: 1. C, 2. Si Kweli, 3. A, 4. Hakuna, 5. Si Kweli, 6. Si Kweli, 7. A, 8. A, 9. Kweli & 10. C

# Habari Kutoka Wilayani

## Arumeru

### Mafanikio ya Utafiti Shirikishi wa Masoko Arumeru

Utafiti shirikishi wa masoko ni mchakato unaotumiwa na wakulima kwa kukusanya na kuchanganua taarifa za masoko na kuzitumia kama nyenzo muhimu katika kuamua ni zao gani walitumie kama chanzo cha mapato. Vikundi 18 ambavyo vinatekeleza Programu ya Kuboresha Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo (AMSDP), vimeshiriki katika zoezi la utafiti shirikishi lililofanyika Februari 14-24, 2005. Baadhi ya masoko yaliyotembelewa ni Kilombero na Kilombero pia walitembelea stoo mbili za Mama Helena na Mzee Ramadhani.

Mchakato huu umewawezesha wakulima kujenga mahusiano na wafanyabiashara, kuelewa mahitaji ya soko, ubora wa mazao, kiasi kinachohitajika sokoni, vipindi vya kuleta mazao sokoni na mfumo wa malipo. Zoezi hili lemeewaongezea wakulima uwezo wao wa kupatania bei ya mazao yao. Wameweza kugundua fursa mpya katika masoko. Wafanyabishara waliwashauri wakulima kutumia mbinu bora wakati wa uzalishaji, uvunaji na uhifadhi ili kuongeza ubora wa mazao yao na kupata faida tarajiwa.

### Wakulima wa Arumeru waomba mafunzo ya usindikaji

TIP hutoa huduma kwa vikundi vilivyo katika maeneo yenye umwagilia wa asili. Kikundi cha Kuhifadhi Mazingira Olgilai (KUMO) ni kati ya vikundi vilivyopata msaada kutoka TIP katika wilaya ya Arumeru. Kikundi kimefanikiwa katika uzalishaji wa mbogamboga na matunda.

Kutokana na ongezeko la uzalishaji wa matunda na mbogamboga, kikundi kinaiomba TIP kutoa mafunzo ya usindikaji yatakayo wawezesha kuongeza thamani kwa mazao yao. Pia kikundi kimeiomba TIP kutangaza mafanikio ya vikundi pamoja na huduma yake kwa jamii kupitima vyombo vya habari.



Mfereji uliokarabatiwa; Skimu ya umwagiliaji ya Nganjoni

## Mwanga

### Wanawake katika Maendeleo Mwanga

Wanawake wana uwezo mkubwa wanapopewa nafasi na ushirikiano katika kuiongoza jamii. Bibi Sofia J. Mruma ni mwenyekiti wa ndiva ya Kampishi wilayani Mwanga. Kikundi kiliingia mkataba na TIP wa kujenga ndiva yao kwa siku 120 kuanzia tarehe 8 Novemba 2005. Kutokana na uwezo wake kiuongozi, kikundi kimefanikiwa kukamilisha ujenzi wa ndiva kabla ya muda uliopangwa. Imewachukua siku 75 tu kukamilisha ujenzi badala ya siku 120. Bi Sofia anasema, "Mafanikio haya yametokana na elimu ya uongozi na mawasiliano tuliyopata kutoka TIP kwa sababu baada ya mafunzo viongozi pamoja na wanakikundi wameelewa majukumu yao katika kikundi.

### Mkulima wa Mwanga aishukuru TIP

*Bi. Janeth Jeremia katibu wa kikundi cha watumia maji cha Kwamjwi atoa shukurani kwa TIP.*

"Tumefanikiwa kukamilisha ujenzi wa ndiva yetu kwa wakati kwa sababu sisi akina mama tumeshirikishwa kikamilifu. Mafunzo ya uongozi, jinsia na ushirikishwaji tuliyopata kutoka TIP yamerahisisha sana kufanikisha ujenzi wa ndiva yetu. Sisi wanawake tumepata fursa ya kuwa viongozi, kumiliki na kutumia rasilimali ya maji na pia kupata mgao sawa na wanaume kwenye ratiba ya kugawa maji. Kabla ya mafunzo kutoka TIP, ilikuwa mwiko wanawake kushiriki katika ujenzi wa ndiva. Tunaishukuru sana TIP kwa huduma yake imesaidia mchango wetu sisi wanawake kuthaminiwa na jamii"

## Same

### Ukarabati wa ndiva waongeza uzalishaji wa tangawizi

Ubora wa maisha ya wanakikundi cha watumia maji wa Maghaeni wilayani Same kimeongezeka baada ya kukamilika ujenzi wa ndiva yao. Kabla ya kujengwa, ndiva yao ilikuwa ina uwezo wa kuhifadhi maji lita 70 za ujazo na baada ya ujenzi uwezo wa kuhifadhi maji umeongezeka hadi kufikia lita 200 za ujazo. Kutokana na ongezeko hili, eneo la umwagiliaji limeongezeka toka hekta 10 – 25 na uzalishaji wa tangawizi umeongezeka toka maguni 10 – 30 kwa robo ekari kwa msimu.

Wakulima hawa wamechagua tangawizi kama zao lao kuu la biashara ambalo lina bei nzuri katika masoko ya ndani na nje. Kwa sasa uzalishaji unafanyika kwa kipindi chote cha mwaka na husadia kuongeza upatikanaji wa chakula.

### Kutumia teknolojia rahisi kwaongeza uzalishaji wa mazao.

Mfumo wa usafirishaji maji ya umwagiliaji kwa njia ya mabomba, ni teknolojia rahisi na yenye gharama nafuu kwa kusafirishia maji ya umwagiliaji toka kwenye chanzo hadi mashambani. Watumia maji wa kikundi cha Heikayu wilayani Same wananufaika na mfumo huu, baada ya kupata msaada wa kuwekewa bomba kwa urefu wa mita 500 toka TIP mwaka 2005. Mzee Zakayo Mgwena amesema, "hakuna upotevu wa maji, kazi zimepungua, hakuna kusafisha mfereji, eneo la umwagiliaji limeongezeka, na kila mwanachama anapata maji na wanatumia mipira kumwagilia mazao"

TIP ni shirika lisilo la kiserikali la Uboreshaji Kilimo cha Umwagiliaji wa Mifereji Asili na Mazingira lililosajiliwa tangu mwaka 1999. Hata hivyo shirika hili lisilo la kiserikali lililoundwa mnamo mwaka 1988, wakati ambao TIP lilianzishwa kama Mpango wa Uboreshaji Mifereji ya Asili chini ya waasisi wa shirika la Maendeleo la Uholanzi (Netherlands SNV).

TIP inashirikiana na Halmashauri za Wilaya ili kuweza kuwafikia kwa urahisi walengwa ambao ni wakulima wa maeneo ya umwagiliaji kwa mifereji ya asili.

Malengo ya TIP ni kuboresha na kuinua viwango vya maisha ya jamii za maeneo ya Tanzania yenye ardhi inayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia mifereji ya asili, kuhifadhi maji na udongo, kustawisha misitu na maeneo ya vyanzo vya maji nchini Tanzania.

TIP inalenga kuhudumia vikundi vidogo vya wakulima (me na ke) vilivyo katika maeneo yenye umwagiliaji Tanzania.

Kifurushai cha TIP
1. Uimarishaji wa vikundi na Jinsia
2. Ushirikishwa wa Matumizi bora ya ardhi
3. Uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji
4. Kuyakabili masoko na uendelezaji wa miradi ya kilimo

SHUKRANI
Shirika la TIP linapenda kutoa shukrani za pekee kwa:
NOVIB, UBALOZI WA JAPANI, UBALOZI WA UHOLANZI na SHIRIKA LA MAENDELEO LA UMOJA WA MATAIFA (UNDP) Kwa ufadhili wa shughuli za TIP

Tuandikie
Tuma maoni yako, mapendekezo, ushauri, hadithi na mawazo yako kwa kutumia anwani ya TIP, andika jina lako kamili na anwani yako

TIP
S.L.P. Box 8909, Moshi - Kilimanjaro
Simu : 027 53025 / 54232
Faksi: 027 51124

Barua pepe: tip@tiptz.org
Mtandao: www.tiptz.org




## Jinsi uboreshaji wa mifereji asili, ulivyoboresha ushirikishwaji wanawake katika shughuli za umwagiliaji

Katika kipindi kilichopita ujenzi wa mifereji kwenye na vyanzo vya maji vilihusishwa na miiko na sheria za kimila. Sheria za kimila hizo ziliwasaidia watu kutokuharibu rasilimali kwa mfano. Misitu, vyanzo vya maji na ardhi. Katika mfumo huu wanaume waliaminiwa kuwa wenye nguvu za kumiliki rasilimali hizo. Sheria hizi zikichunguzwa kwa makini zinaonyesha kwamba zilikusudiwa kumnyima mwanamke mamlaka ya kumiliki rasilimali hizo. Kuni na maji ni mahitaji muhimu kwa watanzania walio wengi, kazi ya kuchota maji na kutafuta kuni ni jukumu la wanawake. Majukumu haya yaliwatia wanaume wasiwasi kwani kuwaruhusu wanawake kutafuta kuni na maji katika misitu hiyo bila ruhusa yao, ingewapa uwezo wanawake kumiliki rasilimali hizo

Kwa hiyo wanaume wakaweka mikakati katika mfumo wa sheria za kimila ili kuzuia wanawake wazitumie rasilimali hizo kama ifuatavyo:

- Wanawake hawakuruhusia kufungua maji kwenye ndiva isipokua mwanaume au mtoto wa kiume. Kama itatokea mwanamke kufungua maji, maisha yake yatakua hatarini na ndiva itabomoka.
- Wanawake hawakuruhusiwa kushiriki katika ujenzi wa vijengo vya umwagiliaji (mfano ndiva), majukumu yao yalikuwa ni kukusanya vifaa vya ujenzi, kuvipeleka karibu na eneo la ujenzi na kumwita mwanaume kuja kuvichukua kupeleka eneo la ujenzi.
- Ili kuonekana wanyenyekevu, wanawake walitakiwa kutozungumza mbele ya wanaume hususani kwenye mikutano kwa hiyo mikutano ya ugawanaji maji ilifanyika kwenye ndiva na vyanzo vya mfereji bila kuwashirikisha wanawake.
- Hapawapo mwanamke kiongozi
- Wanawake hawakuusisha katika kutoa maamuzi.

Ukandimizwaji wa wanawake ulikuwa na madhara yafuatayo:

- Hawakupewa nafasi ya kumiliki rasilimali. Mfano: maji ya umwagiliaji, mapato yatokanayo na umwagiliaji asili, ardhi,miti n.k.
- Kutokuwepo mgawanyo sawa wa kazi. Wanawake walikuwa na mzigo mkubwa wa kazi
- Mgawanyo usio sawa wa mali baina ya mwanamke na mwanaume
- Wanawake hawakuna na haki sawa na wanaume katika kurithi ardhi. Ardhi ilikuwa mali ya mwanaume.
- Kulikuwa hakuna haki katika ndoa

Mafunzo ya jinsia yamesaidia kuepukwa mila zilizokuwa zikimgandamiza mwanamke kutokuwa na haki ya kumiliki na kutumia rasilimali. Wanawake sasa wamehusishwa katika uongozi na kupata mgao sawa wa maji kama wanaume. Hali hii imetokea baada ya TIP kutoa huduma katika maeneo yao.



Wanaume na wanawake kutoka katika kikundi cha watumia maji cha Mshana, wilaya ya Same wakishirikiana kwa pamoja kujenga banio la mfereji wao. Hii ni baada ya kuachana na mila potofu zinazowakataza wanawake kushiriki katika ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji.